
# Kiolesura cha Mtandao wa Chanjo (VINI)

## Jinsi ya Kujisajili na Kuratibu Miadi ya Chanjo ya COVID-19

NH DIVISION OF Public Health Services
Improving health, preventing disease, reducing costs for all
Department of Health and Human Services


Karatasi hii ya Vidokezi ni kuwasaidia wakazi wa New Hampshire kuratibu miadi ya chanjo ya COVID-19 katika Kiolesura cha Mtandao wa Chanjo cha New Hampshire (VINI) Mwongozo huu unaelezea hatua za uchunguzi, usajili na uratibu.




## Uchunguzi na Usajili

Unaweza kuangalia ustahiki wako kwa awamu ya sasa ya chanjo kwa kutembelea www.vaccines.nh.gov na kubofya "*Je, Ninastahiki?*" Au unaweza kufanya uchunguzi kama sehemu ya mchakato wa usajili na uende moja kwa moja kwa "*Jisajili Sasa*" ili kujisajili kwa akaunti ya VINI.

- **Uchunguzi**: Sehemu hii inajumuisha maswali kuhusu umri wako, kazi yako, na hali yako ya kiafya ili kuamua awamu ambayo utastahiki kupewa chanjo.
- **Kukubali Matibabu**: Ikiwa unastahiki katika awamu ya sasa, unapelekwa kwa maswali ya Kukubali Matibabu.
    - Sehemu hii inajumuisha maswali kuhusu athari kali za mzio, tiba ya kingamwili, kupeana kwa chanjo hivi karibuni, hali ya kinga ya mwili iliyoathirika, na ujauzito. Baada ya kujibu maswali haya, utaenda na sehemu ya usajili wa mapema isipokuwa uwe na athari kali ya mzio au ungependa kwanza kujadili na daktari wako.
- **Usajili**: Katika hatua hii katika mchakato, utaulizwa kuweka maelezo yako ya kibinafsi, ambayo yanasaidia kuunda wasifu wako katika VINI.
    - Maelezo haya ni pamoja na Jina, Tarehe ya Kuzaliwa, Jinsia, Mbari, Kabila, Anwani, Habari ya Matibabu, na Bima (hiari). Baada ya kumaliza sehemu zote za lazima, bofya **Wasilisha.**




- **Ukiri wa Barua pepe**: Baada ya kujisajili, utapokea uthibitisho wa barua pepe na kiunganishi cha kuamilisha akaunti yako ya VINI. Barua pepe hiyo itatoka kwa noreply_NHVMS@notices.nh.gov. Ikiwa hutapokea barua pepe ndani ya dakika 10, tafadhali angalia folda yako ya barua taka au piga simu 2-1-1.
    - Kwenye barua pepe, bofya **Amilisha** ili kuingia VINI, ambapo utaunda nenosiri kufikia akaunti yako.
    - Unda nenosiri la akaunti yako na uendelee kuratibu miadi yako ya chanjo ya COVID-19. Kiunganishi cha kuamilisha akaunti yako **kitakwisha muda wake baada ya saa 24**, kwa hivyo tafadhali fungua akaunti yako haraka iwezekanavyo baada ya kupokea barua pepe yako ya kwanza. Ikiwa kiunganishi chako kitaisha muda wake kabla ya kuamilisha akaunti yako, tafadhali piga simu kwa 2-1-1 kuweka upya nenosiri lako.

## Kuratibu Miadi

Mara tu utakapounda nenosiri lako na akaunti, utaona Ukurasa wa Kukaribisha wa VINI. Ili kuratibu miadi ya chanjo ya COVID-19, fuata maagizo yaliyo hapa chini.

# Kiolesura cha Mtandao wa Chanjo (VINI)


## Jinsi ya Kujisajili na Kuratibu Miadi ya Chanjo ya COVID-19

NH DIVISION OF Public Health Services
Improving health, preventing disease, reducing costs for all
Department of Health and Human Services

### Kuratibu Miadi ya Mwanakaya (ikiwa ni lazima)

- Unaruhusiwa kuleta mwanakaya mmoja (1) kwenye miadi yako, ikiwa pia wanastahiki katika awamu yoyote iliyo wazi. Sajili mwanafamilia wako KABLA ya kuratibu miadi yako. Hii imefanywa kwa kubofya **Ongeza Mwanafamilia** kwenye ukurasa wa **Kwanza** wa VINI na kisha kubofya **Ongeza Mwanafamilia**. Utapitishwa kwa Mchakato wa Uchunguzi na Usajili kwa mwanakaya wako. Baada ya kusajili mwanakaya wako, ataweza kuandamana nawe kwenye miadi yako.
    - **Kumbuka**: Ikiwa unasajili mwanakaya wako kupitia mchakato huu, mawasiliano yote yatatumwa kwa anwani ya barua pepe iliyosajili akaunti hiyo katika VINI. Ikiwa mwanakaya wako angependelea kusimamia miadi yake ya chanjo ya COVID-19 na kupokea mawasiliano ya moja kwa moja, tafadhali mwagize akamilishe kwa kujitegemea mchakato wa uchunguzi na usajili kwa kutumia anwani ya barua pepe tofauti na ile iliyotumiwa tayari.

### Kuratibu miadi yako ya kwanza




- Bofya **Unda/Simamia Miadi** kwenye Ukurasa wa Kukaribisha na kwenye skrini inayofuata, bofya **Ratibu Miadi** kwenye kona ya juu ya upande wa kulia wa skrini.
- Chagua **Aina ya Dozi** yako kama **Kwanza**
- Kisha, weka **Anwani** yako au **Msimbo wa ZIP** kutafuta kliniki zilizo katika eneo unayotaka. Orodha ya kliniki zinazofaa vigezo vyako vya utafutaji itaonekana; chagua moja na ubofye **Angalia upatikanaji** ili uone miadi inayopatikana katika eneo hili.




- Baada ya kuchagua kliniki yako unayotaka, chagua tarehe na saa unayotaka. Ikiwa hakuna wakati unaopatikana, tafadhali angalia tarehe nyingine. Baada ya kuchagua saa unayopenda, bofya **Wasilisha**.
    - Ikiwa ungependa kuona miadi inayopatikana kwenye kliniki tofauti, bofya **Badilisha** chini ya Taarifa ya Kliniki upande wa juu kushoto mwa skrini.
    - Ikiwa unataka kubadilisha maelezo yako ya miadi, bofya **Ghairi Miadi** au **Ratibu Upya Miadi**. Kubofya **Ratibu Upya Miadi** kutakurudisha kwenye skrini ambapo unachagua Aina ya Dozi yako. Ukichagua kuratibu upya miadi yako, miadi yako iliyopo itaghairiwa tu baada ya tarehe/saa mpya kuthibitishwa.
- Utaelekezwa kwenye ukurasa ambao unathibitisha miadi yako iliyoratibiwa na kuorodhesha maelezo ya miadi na nambari ya QR. Utahitaji kuleta msimbo wa VINI QR, ambao pia uko kwenye barua pepe yako ya uthibitisho, kwa miadi yako, iwe kwenye kifaa chako cha mkononi au iliyochapishwa.


- Ikitegemea awamu unayostahiki, tafadhali rejelea orodha iliyo hapa chini kwa kile utahitaji pia kuleta kwa miadi yako:
    - **Awamu ya 1A:** Kitambulisho kutoka kwa mwajiri au hati ya mshahara iliyo na jina/anwani na leseni ya udereva au kitambulisho cha asiyekuwa dereva
    - **Awamu ya 1B:** <u>*Mojawapo ya yafuatayo:*</u>
        - Leseni ua udereva au kitambulisho cha asiyekuwa dereva ambacho ni halali na hakijaisha muda wake.
        - Cheki ya mshahara, hati ya mshahara, au mkataba wa ajira unaoonyesha anwani ya kisheria ya New Hampshire, iliyowekwa tarehe ndani ya siku 60 zilizopita.
        - Malipo yaliyotolewa na serikali (yaani, Usalama wa Kijamii), yanayoonyesha anwani ya kisheria ya New Hampshire, iliyowekwa tarehe ndani ya siku 60 zilizopita.

- **Awamu ya 2A:** Leseni ua udereva au kitambulisho cha asiyekuwa dereva ambacho ni halali na hakijaisha muda wake *NA, mojawapo ya yafuatayo:*
  - Cheki ya mshahara, hati ya mshahara, au mkataba wa ajira unaoonyesha ajira yako katika shule, kituo cha utunzaji wa watoto, au kambi ya vijana, iliyowekwa tarehe ndani ya siku 60 zilizopita
  - Barua kwenye karatasi yenye anwani ya shule, kituo cha utunzaji wa watoto, au kambi ya vijana inayosema kuwa unastahiki Awamu ya 2a
  - Kadi ya kitambulisho ya picha iliyotolewa na shule, kituo cha utunzaji wa watoto, au kambi ya vijana
- **Awamu ya 2B:** *Mojawapo ya yafuatayo:*
  - Leseni ua udereva au kitambulisho cha asiyekuwa dereva ambacho ni halali na hakijaisha muda wake
  - Cheki ya mshahara, hati ya mshahara, au mkataba wa ajira unaoonyesha anwani ya kisheria ya New Hampshire, iliyowekwa tarehe ndani ya siku 60 zilizopita
  - Malipo yaliyotolewa na serikali (yaani, Usalama wa Kijamii), yanayoonyesha anwani ya kisheria ya New Hampshire, iliyowekwa tarehe ndani ya siku 60 zilizopita

➢ Taarifa zote za ziada zinazohitajika kwa miadi yako, pamoja na hojaji ambayo unapaswa kujaza kabla ya miadi yako kuokoa muda, zitafika katika barua pepe za ufuatiliaji.

## Kuratibu Miadi Yako ya Pili (ikiwa ni lazima)

Ikiwa unajisajili kwa chanjo ya kudungwa sindano mbili za COVID-19 (Moderna au Pfizer), wafanyakazi wa kliniki wanaweza kuratibu miadi yako ya dozi ya pili unapoondoka baada ya kupokea dozi yako ya kwanza. Miadi hii itaonekana kwenye akaunti yako ya VINI baada ya kuratibiwa. Unaweza pia kuingia tena kwenye akaunti yako ya VINI baada ya kupokea dozi yako ya kwanza ili kuratibu dozi yako ya pili.




Ikiwa unachagua kuratibu miadi yako ya pili mwenyewe, ingia kwenye akaunti yako ya VINI na uchague **Unda na Badilisha Miadi Yangu** na ubofye **Ratibu Miadi**. Chagua ❶ **Aina ya Dozi** yako kama **Pili**. Ikiwa mfumo hautambui maelezo yako, VINI itakuuliza uchague ❷ **Tarehe ya Kupewa Dozi yako ya 1** na ❸ **Jina la Mtengenezaji**. Ikiwa mfumo utatambua maelezo yako, utajaza maelezo haya kimbele. Nafasi za miadi tu ambazo zina mtengenezaji wa chanjo sawa na dozi yako ya kwanza zitaonekana katika utafutaji wako. Angalia hapa chini kwa maelezo kuhusu wakati gani unaweza kuratibu miadi yako ya pili, ikiwa ni lazima.

| Miadi ya Kwanza | | Miadi ya Pili |
|---|---|---|
| Unaratibu miadi yako ya kwanza kwenye kliniki na chanjo ya Moderna COVID-19 mnamo tarehe **1 Machi 2021**. | 28 SIKU | Baada ya kupokea chanjo ya kwanza, mfumo unakuruhusu uratibu miadi yako ya pili mnamo au baada ya tarehe **29 Machi 2021**. |
| Unaratibu miadi yako ya kwanza kwenye kliniki na chanjo ya Pfizer COVID-19 mnamo tarehe **1 Machi 2021**. | 21 SIKU | Baada ya kupokea chanjo ya kwanza, mfumo unakuruhusu uratibu miadi yako ya pili mnamo au baada ya tarehe **22 Machi 2021**. |
| Unaratibu miadi yako ya kwanza kwenye kliniki na chanjo ya Johnson & Johnson COVID-19 mnamo tarehe 1 Machi 2021. | | Hakuna hatua zaidi inayohitajika kwani chanjo za Johnson & Johnson COVID-19 hazihitaji dozi ya pili. |

- Ikiwa unataka kubadilisha au kughairi miadi yako ya pili, unaweza kufikia akaunti yako, bofya **Unda/Simamia Miadi**, na uweke miadi mpya.

**Hongera – umewekea nafasi miadi ya chanjo yako ya COVID-19!**

**Iwapo una maswali yoyote katika mchakato huu, tafadhali piga simu 2-1-1 kwa usaidizi.**